THE MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND TECHNOLOGY
DARMIKI TEACHERS COLLEGE

**AREA "A" KWA WAKOREA**
**S.L.P 4421 DODOMA TANZANIA, SIMU 026 230 0065**
**0752877229, 0658 920 500, 0745 920 520**
**EMAIL ADDRESS: darmikittc@gmail.com**

**Chuo Kimesajiliwa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia - Kwa Usajili Na. CU.155**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU MWAKA 2024/2025 KWA MWANAFUNZI WA KUTWA AU BWENI

## 1. UTANGULIZI

Tunafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi/Awali kwa mwaka wa masomo 2024/2025. Hii ni nafasi ya pekee kwako kwani wengi hawakubahatika kuipata. Chuo kinaendesha Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi na Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali kwa muda wa miaka miwili (2). Ni matumaini yetu kwamba ufikapo hapa Chuoni utaitumia fursa hii vizuri. Chuo cha Ualimu Darmiki kipo katika Mkoa wa Dodoma, Wilaya ya Dodoma Mjini, Area "A" Kwa Wakorea, kata ya Kizota, Jiji la Dodoma. Ni umbali wa kilometa 1 kutoka Dodoma mjini.

## 2. NAMNA YA KUFIKA CHUONI

2.1. Ufikapo kituo cha Mabasi Nanenane, Panda Daladala zinazoelekea Machinga Complex Nauli yake ni kati ya Tsh. 500/= tu halafu chukua bodaboda sh. 1,000. Kwa wale wanaotokea mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara shuka katika kituo cha Daladala Posta halafu chukua boda boda sh. 1,000.

2.2. Wanafunzi wote wanatoka Kanda ya Ziwa pamoja na Mkoa wa Singida, shuka katika Kituo cha Daladala Bahi Road halafu chukua bodaboda sh. 1,000= tu, aidha chuo kina magari madogo kwa kufanya mawasiliano utachukuliwa kituoni.

## 3. KUSAJILIWA CHUONI

Mara ufikapo Chuoni pitia hatua zifuatazo ili kukamilisha usajili wako:

3.1. Onana na mlinzi ili upate maelekezo

3.2. Onana na Msajili wa Wanachuo ili uwasilishe, Vyeti Halisi, Result Slip na nakala zake. Vyeti hivyo ni;

3.2.1. Cheti cha kuhitimu kidato cha nne au sita

3.2.2. Cheti cha kuhitimu mafunzo ya Ualimu (Grade III-A)

3.2.3. Vyeti vya kuhitimu Shule (School Leaving Certificates- kama unacho)

3.2.4. Cheti cha kuzaliwa.

3.2.5. Nakala ya Kitambulisho cha taifa (NIDA)

3.2.6. Onana na Mhasibu wa Chuo ili ukabidhi risiti za Ada na Michango uliyolipia Benki.

3.2.7. Onana na Mkuu wa Chuo ili kukabidhi vifaa

3.2.8. Onana na Mratibu Taaluma ili upangiwe darasa.

3.2.9. Onana na Mwadili wa wanachuo ukaguliwe vifaa na upangiwe bweni kwa mwanafunzi anayekaa Bwenini. NB: Chuo hakitampokea na kumsajili Mwanachuo;

3.2.9.1. Atakayekuja bila vyeti halisi (Originals). Aidha, kwa yeyote atayewasilisha vyeti visivyo halali hatua zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kupelekwa Polisi.

3.2.9.2. Atakayekuwa hajakamilisha malipo ya Ada na Michango. Aidha, kwa wale wanaofadhiliwa na mashirika waje na vithibitisho vyao vyenye saini na muhuri wa shirika/idara husika.

## 4. MAHITAJI MUHIMU KWA WANACHUO

4.1. **SARE**: Wanaume na wanawake waje na mashati 2 ya mikono mirefu ya bluu bahari na tai ndefu nyekundu. Mashati yawe marefu ili uweze kuchomekea vizuri yanapovaliwa.

4.2. Wanaume waje na Suruali bluu nyeusi 2 zenye marinda (Celebration) na mifuko mitatu na mkanda mweusi wa ngozi wenye Bakozi ya saizi ya kati.

4.3. Wasichana washone sketi 2 bluu nyeusi kwa kutumia kitambaa cha suti, ziwe sketi za rinda box mbele tu na ndefu za kuvuka magoti. Watakaotumia hijabu washone sketi bluu nyeusi, shati/nusu kanzu na juba (vyote viwe vya bluu bahari).

4.4. Koti la suti dark bluu linaloendana na suruali au sketi.

4.5. Unatakiwa kuwa na mavazi yasiyozidi matano (05) yenye heshima na hadhi yatakayotumika baada ya vipindi vya darasani na siku za ibada. NB: Nguo za kubana, fupi, zinazoangaza, mipasuo kupita magoti, pensi nyanya, timberland, jeans na nyingine za aina hiyo haziruhusiwi Chuoni. Unatakiwa kuja na begi dogo la kuhifadhia vifaa na nguo zako.

4.6. Uwe na viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi vya kutumbukiza kwa jinsi zote (Me/Ke). Soksi jozi 2 au zaidi nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.

4.7. Uje na; Nguo za michezo: (a) Bukta za blue kwa wanaume na Sketi za solo rangi ya dark blue kwa wanawake. (b) Tracksuit zenye michirizi mweupe (Wanaume iwe ya rangi nyeusi na wanawake iwe ya rangi ya njano.

4.8. Aje na T-Shirt moja rangi nyekundu yenye kola (Form Six).

4.9. Shuka 2 na Blanketi moja mashuka yawe rangi Bluu siyo na marembo yoyote, mto na foronya nyeupe, Chandarua cheupe cha pembe nne chenye ukubwa wa futi tatu kwa sita (ft3 x 6).

4.10. Box File 1 kwa ajili ya kuwekea kumbukumbu binafsi na Rimu mbili (2) za Karatasi za A4, moja ya chuo na nyingine kwa matumizi yako binafsi.

4.11. Mathematical set, daftari kubwa 9 (Counter Book Quire Two Au Three) za kuanzia, rula ya futi moja, Kalamu na penseli za kutosha.

4.12. Aje na kadi ya bima ya afya NHIF na kama huna uje pesa taslimu kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.

## 5. VIFAA BINAFSI

Vifaa vya chakula viwe vya bati au mfupa mgumu, ambavyo ni sahani, bakuli, kikombe, na kijiko (vyombo vya plastiki haviruhusiwi). Godoro, Net ya Mbu, Galoni la kuhifadhia maji ya kunywa na ndoo ya kuogea, mashukana Balnketi, Rimu 1 ya Karatasi, Track suti na Raba na Madaftari. NB: Vyombo vya chakula, ndoo ya kuogea, Godoro na Mashuka ni kwa mwanafunzi anayekaa Bwenini. Aidha, unatakiwa kuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi yako binafsi.

## 6. ULIPAJI WA ADA NA MICHANGO

Unapofika chuoni utatakiwa kutoa risiti mbili za malipo ya Ada na Michango kama ilivyofafanuliwa hapa chini;

| Na | AINA YA MCHANGO | MCHANGANUO WA UTARATIBU WA MALIPO | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Jumla ya Gharama** | **Muhula wa 1** | **Muhula wa 2** | **Muhula wa 3** | **Muhula wa 4** |
| 1. | Ada ya Mafunzo | 1,800,000 | 450,000 | 450,000 | 450,000 | 450,000 |
| 4. | Mafunzo ya Vitendo | 150,000 | - | 75,000 | - | 75,000 |
| 5. | Ada ya Mitihani (NECTA) | 50,000 | - | - | 50,000 | - |
| 6. | Compulsory | 80,000 | 80,000 | - | - | - |

## UTARATIBU WA MALIPO

Malipo ya Ada Yalipwe kwa Awamu Mbili **Sh. 450,000** Muhula kwanza na **Sh. 450,000** Muhula wa Pili. Michango Mingine yote (COMPULSORY) **Sh. 80,000** ilipwe yote muhula wa kwanza, Ada ya Mitihani ya Taifa (NECTA) **Sh. 50,000** italipwa mwaka wa II muhula wa kwanza. Ada ya Mafunzo ya Vitendo (BTP) **Sh. 150,000** italipwa mara mbili **75,000** mwaka wa kwanza **75,000** mwaka wa pili.

Malipo Yote Yafanyike Benki Kwenye Kaunti **Namba 223218000053 Tanzania Commercial Bank - TCB** Jina la Kaunti Ni **Darmiki Teachers College** na Slip ya Bank iwasilishwe kwa Mhasibu wa Chuo. ***Fedha taslimu Haipokelewi!***

## 7. UTHIBITISHO WA AFYA

Unapaswa kupimwa afya yako kabla ya kufika Chuoni na daktari yeyote wa Hospitali inayotambuliwa na Serikali. Iwapo utakuja bila uthibitisho wa daktari udhuru wowote hautapokelewa. Kama unatumia dawa maalum kulingana na maradhi yako uje na dawa zako. Chuo kinatoa matibabu ya huduma ya kwanza tu. Fomu ya kupimwa afya yako imeambatanishwa. Aidha, mwanachuo atahitajika kukata Bima ya Afya ili kuhudumiwa na mfuko wa Bima ya Taifa. Hivyo, mwanachuo anatakiwa aje na kadi yake ya Bima ya afya ya NHIF au kulipia gharama ya Bima ambazo ni **Sh. 50,400/=**.

## 8. SHERIA ZA CHUO

Mwanafunzi atapaswa afuata sheria, kanuni na taratibu zote za chuo kwa muda wote wa mafunzo, sheria hizo zinapatikana kwenye tovuti ya chuo ambayo ni www.darmikittc.ac.tz.

**11. KUFUNGUA CHUO**

11.1. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe 09/09/2024.

11.2. Masomo yataanza rasmi tarehe 16/09/2024. Hakikisha unaingia darasani kwa tarehe hiyo bila kukosa.

11.3. Mwisho wa kuripoti chuoni ni tarehe 23/09//2024.

**12. MOTTO WA CHUO:** "***UFUNGUO WA MAFANIKIO*** "

**13. DIRA YA CHUO** Kuandaa Walimu Walio Bora, Wenye Maadili na Uzalendo, Wanaojali Watu Wenye Mahitaji Maalum, Haki na Wajibu, Kwa Kutumia Sayasi na Technolojia, Kuwa Mstari wa Mbele kulinda Maslahi ya Jamii na Taifa kwa Ujumla

**14. DHAMIRA YA CHUO** Chuo kuwa kituo cha malezi bora kwa vijana wa Kitazania ili kubadiliko Chanya Kitaaluma na Kimaadili ili Kuchochoea Maendeleo kwa jamii na Taifa kwa

Ujumla kwa kutoa mbinu na Ujuzi wa Kukabiliana na Changamoto Zitokanazo na Mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia katika Kuleta Mabadiliko katika kukuza Uchumi.

**JUMUIYA YA CHUO INAKUKARIBISHA CHUONI DARMIKI**
**KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU DARMIKI**

**……………..……………………………………….**
**MKURUGENZI**

CHUO CHA UALIMU
DARMIKI
A Key to Success

**DARMIKI TEACHER'S COLLEGE**

**FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A:** From: Darmiki Teacher's College

To the Medical Officer ……………..…………………..………

Hospital ……………....……………………………………….

Mr./Mrs./Miss…………………….………………...………………………………… (Name in full)

Please examine the above named as to his/her Physical and Mental fitness for a full time Teacher Training Course. The examination should include the following categories [I-II each category or sub category of which will render the applicant ineligible in case of a defect. Primary/Category IV] will also render a girl candidate ineligible for the course:

I. [a] Eye –sight [b] Hearing [c] Limbs [d] Speech [e] Venereal disease [f] Leprosy [g] Epilepsy

II. Neurosis III. Pregnancy (IV) Other serious diseases like TB, HIV, …………….………..…

**MEDICAL CERTIFICATE**

**PART B:** (To be completed by a government medical officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physical fit unfit and mentally fit/unfit for a full time teacher training course.

I. [a] Eye-sight………….. [b] Hearing…….……… [c] Limbs……….. [d] Speech………

[e] Venereal disease……………….. [f] Leprosy……………. [g] Epilepsy……….…..…

II. Neurosis ……………………………………………………………......……………………..

III. Serious diseased………………………………………………………………………………….

IV. Pregnancy ……………………………………………………...……………………….…..

Name…………………………….…... Signature……………………….. Date………………………

Designation ………………………………….……..... Station …………………..…………..……

***Official Stamp:***